## NAMBA 4: MARKO 6:30-44: YESU AWALISHA WATU ELFU TANO:

Katika kipindi hiki, tunakwenda kujifunza moja ya vifungu katika injili ya Marko, hivyo tafadhali turejee pamoja nami katika injili ya **Marko sura ya sita**. Hii ni sura yenye shughuli na mambo mengi sana! Yesu alikuwa Nazareti, na siku ya Sabato alikuwa akifundisha katika sinagogi - lakini watu walimkataa. Kwa kweli tunaambiwa katika **mstari wa tatu** kwamba, walimwona kuwa ni mwenye makosa. Swali walilouliza ni hili: *"Anawezaje mtu huyu, ambaye alikuwa seremala tu wakati alipoishi hapa Nazareti, kufundisha kwa mamlaka kama hayo"?* Walimkataa, na Yesu alishangazwa nao kwa kukosa imani naye. Yesu aliwatuma wanafunzi wake kumi na wawili kwa ajili ya kufanya huduma. **Mstari wa saba** unatuambia kwamba aliwapa mamlaka kuwaponya wagonjwa na kuwafukuza pepo wabaya, na aliwaambia wahubiri ujumbe wa toba.

Wakati ambapo wanafunzi walikuwa wameenda mbali, Yesu alijua dhahiri kwamba **Yohana Mbatizaji** alikuwa ameuliwa na **Herode** – na tunajua habari ya jinsi Yohana alivyouawa kwa kukatwa kichwa chake wakati akiwa gerezani. Marko hatuambii haya, lakini Yesu aliposikia habari hiyo, alifadhaishwa. Yohana alikuwa akiitayarisha njia kwa ajili ya Yesu kufanya huduma yake, na pia alikuwa ndugu yake kifamilia. Yohana alikuwa na uhusiano na Yesu. Kumbuka, mama yake **Mariamu** alikuwa binamu wa mama wa Yohana wa Elizabeti. Kwa hivyo Yesu alifadhaika aliposikia kwamba Yohana alikuwa ameuawa. Alitaka kuondoka atoke katika umati. Alitaka kwenda mahali fulani penye utulivu ili aweze kuomboleza. Hivyo basi, hebu tusome ili tuone kinachotokea baadaye. **Marko sura ya sita, mstari wa thelathini hadi arobaini na nne.**

Tunaweza kuona kwamba wanafunzi walikuwa na shughuli nyingi sana, na katika **mstari wa thelathini na moja** Yesu akawaambia: "*Twendeni mahali pa utulivu, na tupate kupumuzika".* Yesu anawajali wanafunzi wake. Tunaambiwa kuwa hapakuwa na nafasi hata ya kula, kwa sababu watu wengi walikuwa wakitaka kumwona Yesu. Na hivyo waliingia kwenye mashua na **mstari wa thelathini na mbili** unatuambia kwamba, walisafiri kwenda mahali pa faragha, ili waweze kuwa wao wenyewe tu. **Luka** anatuambia kwamba mahali hapo palikuwa ni karibu na **Bethsaida**, kaskazini mwa ziwa Galilaya. "*Twendeni – tupate kupumuzika*". Yesu alikuwa amechoka. Wanafunzi wake pia walikuwa wamechoka. Walihitaji muda wa kupumuzika; walihitaji likizo. Wakati mwingine katika maisha yetu pale tunapokuwa na shughuli nyingi, ni vizuri kuwa na likizo, na kwenda mbali kwa ajili ya kujituliza na kupumuzika. Ninajua baadhi yenu wachache wenu mmechukua muda wenu wa huduma, na mmeshakaa katika kituo cha Mapumziko cha Sanga Sanga.

Hilo ni jambo la busara sana kulifanya. Huu ni muda wa kupumzika; muda wa kulala; muda wa kuomba; muda wa kuzungumza; muda wa kusoma Biblia yako; wakati wa kufikiri na kutafakari, bila ya kupata usumbufu wa huduma. Kuchukua na kutumia muda kwa namna hii, ni kitu kizuri kwa ajili ya nafsi, na kitu kizuri sana kwa ajili ya mwili. Yesu na wanafunzi walihitaji kufanya hivyo.

Lakini – wakati mashua yao ikiwa bado hata haijafika mahali ilipokuwa ikielekea, umati wa watu ulikuwa tayari umeshakusanyika na ulikuwa unamsubiri kumwona Yesu. Katika kipindi hiki Yesu alikuwa mtu maarufu sana. Watu walikimbia kutoka miji na vijiji vya karibu na ziwa, ili waje kukutana na Yesu. Je, jibu la Yesu ni lipi? Na Je, jibu lako lingekuwa ni nini? Kama mimi ni mwaminifu, ningewaambia watu hawa kuwa: '*Nendeni mbali; niacheni peke yangu, kwa sababu ninahitaji muda wa kuwa peke yangu".* Lakini Yesu hakusema hivyo. Angalia

katika **mstari wa thelathini na nne**: "*wakati Yesu aliposhuka na kuuona umati mkubwa, aliwahurumia kwa sababu walikuwa ni kama kondoo wasio na mchungaji. Basi akaanza kuwafundisha."* Badala ya kuwakasirikia, alikuwa mvumilivu kwao; kwa kweli aliwahurumia.

Sasa, neno hili '*huruma*' lina nguvu sana maana limetumiwa **mara tisa** katika injili. Kama ukiangalia nyuma katika **sura ya kwanza, mstari wa arobaini na moja** utaona kwamba, mtu mwenye ukoma alimwendea Yesu; alikuwa na ugonjwa mbaya wa ngozi. Alimwendea Yesu na kupiga magoti mbele yake, na alimsihi Yesu amponye. Je, Yesu alimjibuje? *"Akiwa amejawa na* ***huruma****, Yesu aliuonyosha mkono wake na kumgusa yule mtu".* Yesu alipomwona mtu, alimwonea huruma. Alikuwa na huruma. Ni neno lile lile limetumika hapa katika **sura ya 6, mstari wa thelathinii na nne.** Aliuangalia umati na kuuonea huruma. Lakini neno la Kigiriki ambalo limetumika hapa '*huruma*' ni neno lenye nguvu sana, ambalo kwa kweli linatokana na neno sawa na '**tumbo'**.

Sasa, hiyo inaweza kuonekana kama ajabu kwa mara ya kwanza. Ni kwa namna gani neno '*tumbo*' lina uhusiano wowote na huruma? Lina maana kwamba Yesu alijisikia huruma kwa watu hawa hapa, katika tumbo. Ina maana kwamba alijisikia maumivu kwa watu hawa, si tu katika akili yake, lakini pia katika mwili wake. Yeye alisukumwa ndani ya mwili wake na huruma kwa ajili ya watu hawa. Alijisikia hapa hapa katika tumbo lake. Wakati mwingine, tunapoona kitu ambacho ni cha kutisha, kinaweza kutufanya tujihisi wagonjwa. Kile tuna-chokiona kwa macho yetu kinaweza kusababisha maumivu ndani ya kimwili katika tumbo letu. Kama mtu akikupiga katika tumbo, atakufanya ulie.

Ilikuwa kama hivyo. Yesu alipowaona, ilikuwa kama amepigwa katika tumbo lake, na alitaka kulia kwa uchungu, kwa sababu ya kile alichokiona. Kwa nini Yesu alijisikia hivyo? Haikuwa kwa sababu walikuwa wagonjwa au wenye njaa, ilikuwa ni kwa sababu ya hali yao ya kiroho. Walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji.

Walikuwa wamepotea katika hali ya kiroho. Hapakuwa na mtu wa kuwaongoza. Katika Tanzania, utaona wachungaji wakichunga ng'ombe zao, au mbuzi zao. Wachungaji hujitahidi kuwazuia mifugo yao isiende kwenye barabara. Wanajitahidi kuwalinda dhidi ya hatari. Wanawaongoza kwenye maji, ili waweze kunywa maji. Huwaongoza kwenye maeneo ambayo wanaweza kupata majani ya kula. Na kisha mwisho wa siku, wanawarudisha wanyama hao nyumbani, na huwaingiza katika boma, ili kuwalinda dhidi ya wezi na wanyama wakali wa porini. Je, waweza kufikiria ni kitu gani kitatokea kama Mchungaji atakimbia? Ng'ombe watasambaa na kuingia barabarani, na wanaweza kugongwa na magari. Huenda mbuzi wanaweza kutangatanga na kwenda mbali. Labda wangeweza kupotea.

Hii ilikuwa ni sawa kama ilivyokuwa kwa watu wa Israeli kwa wakati huu. Hawakuwa na viongozi wema wa kiroho. Hawakuwa na mtu wa kuwaongoza au kuwalinda. Lakini, hiki hakikuwa kitu kipya. Jambo hili limekuwa likitokea kwa miaka mingi, hata huko nyuma katika siku za Agano la Kale. **Miaka mia sita** Kabla ya Kristo, kulikuwa na nabii aitwaye **Ezekieli**. Alikuwa akiongelea kuhusu tatizo hilo hilo. Kupitia kwa Ezekieli, Mungu alizungumza na watu, ambao walikuwa wamemaanishwa kuwa viongozi; watu hawa walikuwa ni makuhani na viongozi wa kidini. Watu hawa walikuwa hawafanyi kazi zao ipasavyo, na Mungu hakuwafurahia kabisa. Hebu tusome kile alichokiandika katika **Ezekieli sura ya thelathini na nne, mstari wa mbili hadi wa tano**. *"Ole wao wachungaji wa Israeli ambao wanajilisha wao wenyewe! Je, haiwapasi wachungaji kulilisha kundi? Mnawala walionona, mnajivika manyoya na mnachinja walionona, lakini hamwalishi kondoo. Wagonjwa hamkuwatia nguvu, wala kuwaponywa wenye magonjwa, wala hamkuwafunga waliovunjika. Wala*

*hamkuwarudisha waliopotea. Bali mmetawala kwa ukali na ukatili. Nao wametawanyika kwa sababu hapakuwa na mchungaji".*

Hapa katika **Marko sura ya sita** hali ya Israeli ilikuwa haijaboreshwa, hata baada ya miaka **mia sita**. Watu walikuwa bado wamepotea kiroho. Mafarisayo na viongozi wa dini, walikuwa hawajafanya chochote katika kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa Masihi. Walikuwa wameliacha kundi hilo, na walikuwa hawawaongozi watu wao vizuri. Na Yesu alipolitazama kundi hili kubwa la watu aliwaonea huruma. Kwa nini?

Kwa sababu walikuwa wamepotea kiroho, na walikuwa hawana msaada. Nina maswali mawili kwa ajili yako. Kama mchungaji au mwinjilisti, Je, unayo huruma kwa watu wale, ambao wamepotea kiroho? Je, unakumbuka mara ya mwisho ambapo uliona huruma yenye nguvu, ndani yako, kwa sababu ya mtu ambaye hamjui Kristo? Je, tunawajali watu waliopotea?

Kuna mamilioni ya watu ambao wanakufa bila Kristo. Wengi wao hawajawahi kusikia kwamba Yesu alikufa kwa ajili yao. Sikiliza takwimu hizi – na iache iingie na kuzama katika akili yako. Idadi ya watu ambao hawajawahi kuisikia injili: watu **milioni mia nane sitini na tano** ni wa Waislamu; **milioni mia tano na hamsini** ni Wahindu; **milioni mia mbili na sabini na tano** ni Wabudha. Watu **milioni mia moja na arobiani** kutoka zaidi ya makabila **elfu Mbili mia tano** huamini dini za asili. Watu hawa hawajawahi kuisikia injili! Je, tunajisikiaje kuhusiana na hilo? Baadhi ya watu hao wanaishi katika jamii zetu. Je, tunajali kuwa watu hawa wanakwenda jehanamu? Je, tunahurumia watu hawa ambao wamepotea waliomo katika jamii zetu? Je tunafanya nini katika makanisa yetu? Kama kiongozi, Je, unajaribu kulisaidia kanisa lako katika kuwafikia watu waliopotea? Je, unatenda kwa huruma kwa wale ambao hawamjui Kristo?

Swali la pili ambalo nataka kuuliza ni hili: Ezekiel alizungumzia juu ya wachungaji wabaya. Yesu aliongelea kuhusu wachungaji wabaya. Kama mchungaji, Je, wewe ni mchungaji mwema, au mchungaji mbaya? Tuliongea kuhususiana na hili miaka miwili iliyopita, wakati tulipoiangalia Barua ya Kwanza ya Petro. Je, unakumbuka? **Sura ya tano, mstari wa mbili** inasema *"Lichungeni kundi la Mungu lililo chini ya uangalizi wenu, mkihudumu kama waangalizi*." **Sura ya tano, mstari wa tatu** inasema: "*Uwe mfano mzuri kwa kundi lako*". Kama wewe ni mchungaji hapa leo, umepewa jukumu la kuliongoza Kanisa lako. Unawajibika kuboresha afya ya kiroho ya washirika wako. Huo ni wajibu mkubwa! Je, wewe ni mchungaji mzuri, au mchungaji mbaya? Je, unalilisha kundi lako chakula kizuri, au chakula kibaya? Je, unalijali kundi lako? Je, wewe ni mfano mzuri kwa kundi lako – au uko kama wachungaji wa Agano la Kale, Je, umewacha bila kuwajali washirika wako?

Cha kusikitisha leo, kuna baadhi ya wachungaji ambao hawalijali kundi lao kabisa - lakini badala yake wanahakikisha kwamba wanajijali wenyewe kwanza. Hawalilishi wala kuliimarisha kundi lao. Hawawezi hata kuwatafuta wale waliopotea, na kuwatawala kwa ukali na ukatili. Natumaini wewe si mmoja wa wale wachungaji, kwa sababu kama na wewe uko hivyo, kanisa lako litakuwa na afya mbaya ya kiroho, na siku moja, utatoa hesabu ya matendo yako kwa Mchungaji Mkuu - Bwana Mungu Mwenyezi.

Yesu aliwahurumia watu hawa – na hivyo, katika **mstari wa thelathini na nne**, akaanza kuwafundisha mambo mengi. Yesu aliwataka wajifunze. Alitaka kuwafundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Alitaka kuwalisha kiroho – hili ilikuwa ni jambo muhimu kwake. Lakini tambua kile

kilichotokea baada ya kuwapa chakula cha kiroho; pia aliwapatia chakula cha kimwili kwa ajili ya miili yao.

Na bila shaka tunajua yote kuhusu kitendo cha kulisha ya watu **elfu tano**. Ni muujiza maarufu. Watu wangapi walilishwa? Angalia katika **mstari wa arobaini na nne**. *"Idadi ya watu ambao walikuwa wamekula walikuwa 5000".* Lakini Marko aliwahesabu wanaume tu – sio wanawake na watoto. Ukisoma kuhusu muujiza huu katika injili ya Mathayo, utaona anasema hivi: "*idadi ya wale ambao walikula ilikuwa ni takribani watu **elfu tano**, pasipo wanawake na watoto*" (Mathayo 14:21). Hakuna injili yoyote ambayo iliwahesabu wanawake au watoto – lakini lazima walikuwa hapo pia. Hivyo, huenda ni vizuri sana kama tukiuita muujiza huu: kulishwa kwa watu **elfu kumi**! Pengine Yesu aliwalisha watu elfu kumi hapa – na aliweza kuyafanya haya kwa vipande vitano tu vya mikate, na samaki wawili wadogo. Je, jambo hili lilitokeaje?

**Mstari wa thelathini na tano** unatuambia kuwa muda wa siku ulikuwa umeendelea sana – ilikuwa yapata saa kama **kumi** za mchana. Kulikuwa kumebakia masaa **matatu** ya kabla ya giza kuingia. Na wanafunzi walimwendea Yesu, na wakapendekeza kuwa awatume makutano - ili waweze kwenda kujinunulia chakula, kabla ya giza halijaingia bado. Labda walikuwa wanawajali watu, au labda walitaka wabaki wao tu wenyewe! Lakini Yesu akawaambia katika **mstari wa thelathini na saba**: "*Wapeni ninyi chakula*". Hili lilikuwa ni jaribio la imani yao, lakini Je, walimwambia nini Yesu? Kwa kweli, hawaonyeshi hali kumheshimu katika jibu lao, kwa sababu walimwambia: "*lazima utakuwa unatania! Je, unadhani tutatumia fedha zote hizo kununua mikate? Itagharimu mshahara wa miezi **minane** kufanya hivyo* "! Je, hiyo ni kama shilingi ngapi kwa fedha ya Tanzania leo?

Sijui mshahara wa wastani wa Tanzania ni kiasi gani, lakini ikiwa mtu analipwa shilingi **elfu kumi** kwa kila siku, kwa kipindi cha miezi **minane**, jumla yake ni shilingi **milioni mbili na laki nne**. Ikiwa mtu analipwa shilingi **elfu tano** kwa siku kwa miezi minane, jumla itakuwa ni shilingi **milioni moja na laki mbili**. Hiyo ni fedha nyingi! Hiyo ni nyingi kwa mikate! *Je, unaweza kufikiria namna ya kutumia fedha yote hiyo kununua mikate, kwa ajili ya kulisha watu **elfu kumi**?!* Wanafunzi wakamwambia Yesu, hatuwezi kumudu kununua chakula cha watu hawa wote.

Kwa hiyo, katika **mstari wa thelathini na nane** Yesu akawaambia: "*Mna mikate mingapi*"? Na kisha akawaambia waende katika makutano ili kujua ni kiasi gani cha chakula kilichopo. Walirudi kwake, na kumwambia kuwa wamepata "*mikate mitano, na samaki wawili tu".* Je waliipata wapi hiyo? Marko hatuambii – lakini Yohana anatuambia hivyo. Kwa kweli Yohana anatuambia katika **Yohana sura ya sita, mstari wa tisa** ya kwamba **Andrea**, ndugu ya Petro, alimkuta mvulana aliyekuwa na mikate mitano, na samaki wawili wadogo.

Angalia neno '*wadogo*' katika kifungu hicho. Hawa hawakuwa samaki wakubwa, bali walikuwa ni wadogo. Hata mikate ilikuwa ni midogo. Hiki kilikuwa ni chakula cha kumtosha mtu mmoja, au labda watu wawili - lakini huyu mvulana mdogo, ambaye jina lake halijatajwa, alikuwa na furaha ya kushiriki chakula chake cha mchana pamoja na Yesu! Na nitarejea katika suala hili, baada ya dakika chache, kwa sababu tunaweza kujifunza kitu muhimu hapa. Kwa hiyo, Yesu anafanya nini? Angalia **mstari wa thelathini na tisa**. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wahakikishe kwamba, watu wamekaa chini kwenye nyasi, katika makundi ya watu **hamsini** na **mia**. Kwa maneno mengine, alitaka watu wapangwe vizuri. Yeye hakutaka watu kuwa shagalabagala!! Hataki watu kuleta msongamano mbele zake. Anataka mambo yawe katika

hali ya utulivu na utaratibu, na watu wakiwa wamekaa chini, ili kusubiri kupokea chakula. Na kwa njia hii, pia itakuwa rahisi kwa wanafunzi kusambaza na kugawa chakula.

Marko pia anatuambia kuwa watu walikaa chini kwenye majani za kijani. Je, hiyo ina maana gani? Inatuambia ni wakati gani wa mwaka muujiza huu ulitokea. Pengine ulikuwa mwezi wa Machi au Aprili, kwa sababu ndio wakati kuna majani mengi ya kijani. Kuanzia Mei hadi Novemba katika Israeli, kuna joto sana. Nyasi hufa kwa sababu ya ukosefu wa mvua. Kwa kweli nyasi huwa za kahawia, na njano, wakati huu wa mwaka, lakini mwezi Machi na Aprili, baada tu ya kunyesha kwa mvua, huwa kuna nyasi nyingi za kijani juu ya ardhi.

Na kisha katika **mstari wa arobaini na moja**, kabla ya Yesu hajauvunja mkate, aliinua macho yake, na akaangalia juu mbinguni, na kisha akamwomba Baba yake. Anamshukuru Mungu kwa chakula. Anasema neema. Hiki ni kitu ambacho Wakristo wengi wanakifanya kabla ya kula chakula. Tunamshukuru Mungu kwa kutupa chakula chetu. Tunatambua kwamba kila kitu tulicho nacho kimetoka kwa Mungu – na kwa hivyo tunataka kumwambia Mungu 'asante' kwa ajili ya zawadi yake aliyo-tupatia. Kwa Wayahudi, walikuwa na sala ya kijadi, au baraka, ambayo walikuwa wakiitumia kabla ya mlo: ni sala fupi sana: *"Ubarikiwe wewe Ee Bwana, mfalme wa ulimwengu, ambaye huleta mkate kutoka duniani".* Na labda, kama Yesu alipomaliza kumshukuru Mungu kwa mkate huu, na samaki, aliisema sala hii. Hatujui, kwa sababu Biblia haituambii hivyo. Jambo muhimu la kutambua hapa ni kwamba, alimshukuru Baba kwa ajili ya chakula. Na huenda pia alimwomba Mungu ili amsaidie kuufanya muujiza huu.

Na kisha, kwa namna fulani, mikate na samaki wakaongezeka - na badala ya mikate mitano tu, na samaki wawili; badala ya chakula kidogo cha mchana cha kijana mdogo - kuna maelfu ya vipande vya mikate na samaki! Kuna chakula zaidi ya kile kilichohitajika kulisha kundi hili kubwa. Marko anatuambia katika **mstari wa arobaini na mbili** kuwa "wote *walikula na kushiba".* Kila mtu alisema "*Mimi nimeshiba kweli*"! Kulikuwa na chakula kingi sana maana kila mtu alikula vya kutosha. Kwa kweli, tunaambiwa katika **mstari wa arobaini na tatu**, baada ya mlo, wanafunzi "*walikusanya vipande vya mikate na samaki vikapu **kumi na mbili** vilivyojaa*". Wakati kila mtu alipomaliza kula, na huku wanafunzi walikuwa wakifungasha na kuweka mambo sawa, walikuta kulikuwa na mabaki ya chakula. Utabaini kuwa kulikuwa vikapu **kumi na mbili** vya chakula vilivyobaki; kikapu kimoja kwa kila mwanafunzi. Yesu alitoa chakula kingi sana, ili kwamba hata na wanafunzi wapate chakula kwa siku chache zijazo pia! Alitoa chakula kwa ajili ya makutano, lakini pia alitoa kwa ajili ya wanafunzi wake.

Hapa kuna swali - ingawa silijui jibu lake! Je, unafikiri kwamba kila mtu katika umati ule alijua kuwa huu ulikuwa ni muujiza? Wanafunzi walijua hivyo kwa sababu walikuwa wakisambaza chakula. Walijua kuwa kulikuwa na mikate **mitano** tu, na samaki **wawili** wadogo. Labda wanafunzi hata waliweza kuona chakula kikizidishwa mbele ya macho yao. Nina uhakika kuwa walishangazwa sana. Lakini, kwa watu waliokuwa wamekaa mbali na Yesu, labda hata hawakujua kuwa huu ulikuwa muujiza. Hatujui kwa uhakika.

Kabla ya kuhitimisha, ningependa tuangalie kwa ufupi njia mbili, ambazo zinaweza kutusaidia kutumia baadhi ya mafundisho haya, katika maisha yetu. **Kwanza,** tambua kwamba Yesu alitaka kumjum-uisha mvulana mdogo katika muujiza huu. Marko hatuambii kuhusu mvulana mdogo – Yohana ndiye pekee anayetuambia hivyo. Lakini tunaambiwa katika **mstari wa thelathini na nane**, kwamba Yesu aliwauliza wanafunzi, ili watafute ni chakula kiasi gani kilichokuwa kwenye umati. Kwa nini? Kwa nini alihitaji vipande **vitano** vya mikate na samaki

**wawili** wadogo? Jibu ni hili – Yesu alikuwa hana haja navyo! Kama angelivitaka, Yesu angeweza kutoa mikate na samaki, bila hata kutumia chakula cha mchana cha mvulana mdogo. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu! Yeye alikuwa anaweza kufanya yasiyowezekana. Aliwaponya watu ambao walikuwa wagonjwa. Alikuwa na uwezo dhidi ya pepo wabaya. Alikuwa na nguvu juu ya upepo na mvua. Yeye alikuwa na nguvu juu ya uumbaji. Tunajua hivyo kutoka katika kitabu cha **Mwanzo sura ya kwanza**. *"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa tena utupu".* Bado, Mungu aliweza kuumba mimea, na miti, na wanyama, bila kutumia kitu chochote! Yeye ana uwezo wa kufanya hivyo. Hivyo, kwa nini Yesu hakufanya muujiza tu, na kuzalisha mikate na samaki, bila kutumia chakula cha mchana cha mvulana mdogo? Ninafikiri hii inaonyesha kwamba, Yesu anataka kututumia katika kuujenga ufalme wake. Yeye anatutaka sisi, kama watoto wake, kushiriki katika kazi yake. Hakuhitaji mchango wowote kutoka kwa mvulana mdogo, lakini alichagua kutumia kile ambacho mvulana huyu alikuwa nacho, kama sehemu ya muujiza. Hili ni jambo la ajabu!

Tunatakiwa kuelewa kwamba, Mungu anataka kututumia sisi ili kusaidia kuleta mkate kwa watu wenye wahitaji. Mimi sizungumzii juu ya mkate halisi, kwa ajili yetu kula - bali ni mkate wa kiroho. Yeye anataka kututumia sisi - wewe na mimi, katika kuleta msaada kwa ulimwengu. Yeye anatutaka sisi kuhusika katika kuushirikisha Mkate wa Maisha katika ulimwengu tunaoishi. Na ninaposema *'mkate wa uzima'*, ninamaanisha Yesu. Anatutaka tuushirikishe ulimwengu habari za Yesu. Je, unafikiri kuwa Yesu anatuhitaji sisi tuifanye kazi yake? Je, unafikiri kuwa Yesu anahitaji usaidizi katika kujenga ufalme wa Mungu? La hasha! Hapana Kabisa! Yeye hatuhitaji sisi. Anaweza kufanya hivyo bila sisi, kama vile tu ambavyo angeweza kuufanya muujiza, bila kutumia mikate mitano na samaki wawili. Kumbuka, kabla Yesu hajapaa mbinguni, aliwaamuru wanafunzi wake akisema, *"enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi".* Je, unafikiri kwamba ni kweli Yesu aliwahitaji wanafunzi kufanya hivyo? Je, unafikiri kuwa Yesu angeweza kufanya hivyo yeye mwenyewe? Bila shaka angeliweza. Yesu angeweza kulijenga Kanisa yeye mwenyewe – lakini alichagua kufanya kazi kupitia kwa wanafunzi ili kulijenga Kanisa la kwanza.

Na hata leo, Mungu amechagua kututumia wewe na mimi katika kazi yake. Kama Mchungaji; kama Mwinjilisti; kama Mwalimu wa Biblia, anatuchagua ili tushiriki katika kazi yake. Yeye anataka kutujumuisha sisi katika kazi yake, ingawa wakati mwingine tumeshindwa kufanya kazi pamoja naye. Je, hiyo si ajabu? Hebu nisome mstari kutoka Waraka wa Pili kwa **Wakorintho**, ambao unatuonyesha kwamba Yeye anataka kufanya kazi kupitia kwetu. **Sura ya tano, mstari wa ishirini** inasema: "*Yeye ametupa sisi ujumbe wa upatanisho. Kwa hiyo, sisi ni wajumbe wa Kristo, kana kwamba Mungu alikuwa akiwasihi ninyi kupitia kwetu".* Yesu alitaka kumtumia mvulana mdogo katika muujiza wake, kama vile anavyotaka kututumia wewe na mimi, katika kuujenga ufalme wake. Asante Bwana kwa kuwatumia watu wadogo! Pili, tunajifunza kwamba Mungu anaweza kutumia kitu ambacho ni kidogo sana, pale kinapowekwa na kukabidhiwa kwake. Je, unaweza kufikiria wanafunzi wakitembea na kuzunguka katika umati wa watu, na kuwauliza chakula ambacho walikuwa nacho? Walirudi kwa Yesu na kusema: "*tumeweza kupata tu vipande vitano vya mikate, na samaki wawili wadogo".* Je, kiasi hiki kidogo cha chakula, chaweza kulisha watu hawa wote? Ni kiasi kidogo tu, kinaweza kumlisha mtu mmoja, au wawili. Wakati mwingine tunaweza kufikiri kwamba kile tunachopaswa kumpa Mungu ni kidogo sana. Unaweza kufikiri kwamba mchango wako ni mdogo sana, katika ujenzi wa ufalme wa Mungu, na ya kwamba si kitu cha thamani hata kukitoa. Unaweza kufikiri kwamba huwezi kufanya chochote kwa ajili ya Mungu, kwa sababu huna kanisa kubwa sana, au huna pesa nyingi. Unaweza kufikiri kwamba wewe ni mtu mdogo tu katika ufalme wa Mungu. Ni kitu gani naweza kukitoa ili kuleta tofauti? Mletee Mungu kile ulicho nacho - si kile usichokuwa nacho. Toa chakula

chako kidogo cha mchana, kama mchango wako! Mtolee kile alichokupa, kwa sababu kama ukitoa kwa moyo wa dhati, atakitumia ulichokitoa katika kujenga ufalme.

Je, unafikiri mvulana huyu mdogo alidhani kuwa mchango wake, ungekuwa na manufaa kwa Yesu? Hapana! Nina hakika alishangaa kuona namna Yesu alivyokifanyia kile chakula chake kidogo cha mchana! Unaona, hata kama unafikiria sadaka yako ni ndogo sana, itakushangaza kuona kile ambacho Mungu anaweza kufanya kupitia mchango huo. Mchango wetu kidogo haufai kitu katika mikono yetu, lakini pale tunapompa Yeye, anaweza kuzidisha, na kufanya mambo kuwa makubwa zaidi kuliko tunavyoweza kufikiria. Kama ukimpa zawadi yako, yeye ataya-zidisha ili kuwa kitu kikubwa zaidi kuliko.

Hicho ndicho tunachojifunza tunapoisoma Biblia. Kuna mifano mingi mahali ambapo Mungu anatumia maisha, ambayo hayakuwa ya muhimu katika kazi yake. **Daudi** alikuwa ni mvulana mdogo. Alikuwa mchungaji tu - lakini alikuwa mfalme juu ya Israeli. **Gideon**i alikuwa mtu ambaye hakuwa wa muhimu katika kabila lake, lakini Mungu alimtumia kwa nguvu katika kuwashinda Wamidiani. **Mariamu** alichaguliwa kuwa mama wa Yesu, lakini alikuwa ni msichana mdogo na mkulima huko Nazareti. Katika jamii yake hakuwa mtu wa muhimu, au aliyejulikana sana, lakini kwa sababu alikuwa tayari kutumiwa na Mungu, Masihi alizaliwa kwake, na kuubadilisha ulimwengu! Baada ya kifo na ufufuo wake, wakati ule Yesu alipopaa kwenda mbinguni, aliondoka na kuacha kikundi kidogo cha wanafunzi, ili kufanya kazi yake – na baada ya miaka **elfu mbili**, kanisa ni kubwa sana!

Kuna mamilioni ya Wakristo duniani. Je, unadhani kuwa wanafunzi walifikiri kuwa kazi yao ingekua kuwa kubwa sana? Nina shaka. Lakini waliyatoa maisha yao madogo kwa Mungu, naye aliyatumia kulijenga Kanisa lake. Waliyakabidhi maisha yao kwa Mungu, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ndani yao, waliweza kuubadilisha ulimwengu! Aisee! Hebu tukumbuke kwamba Mungu anataka kuwatumia watu wa kawaida tu, kama wewe na mimi. Yeye hukigeuza kile kilichotolewa kwake, na kukifanya kuwa kitu maalumu. Anavichukua vipande **vitano** ya mikate, na samaki **wawili** wadogo, na akavizidisha na kuwa maelfu ya mikate, na maelfu ya samaki! Kwa njia hiyo hiyo, anaweza kukichukua kile tulichompa, na kukibadilisha kuwa kitu chenye nguvu sana, kwa ajili ya kujenga ufalme wake. Amina.